

Maswali

1. Wakati wa chakula cha Pasaka Yesu aliambia Petro nini?
2. Baada ya Yesu kukamatwa, Petro alifanya nini?
3. Mbona alifwata?
4. Wakuu wa Makuhani walipeleka Yesu wapi?
5. Petro alifanya nini ndani ya uwanja wa mahakama makuu?
6. Kijakazi alimuuliza Petro nini alipomwona kwa mwangaza wa moto?
7. Petro alimjibu eti nini?
8. Nini ilfanyika baada ya Petro kukana Yesu mara tatu?
9. Petro alijihisi namna gani?

Majibu

1. Kwamba kabla jogoo awike, Petro atamkana mara tatu
2. Petro alifwata Yesu kwa umbali nyuma ya walinzi
3. Petro alitaka awe karibu na Bwana wake.
4. Kwa mahakama makuu ya Wayahudi.
5. Alienda kwa moto ili aote.
6. Kijakazi alimuuliza Petro, “Wewe ni rafiki wa huyo mtu aliyekamatwa?”
7. “La la umekosea.” Petro alijibu.
8. Jogoo aliwika.
9. Petro alijuta kwa kufanya hivyo na akalia.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 2

45 Petro anamkana Yesu

Marejeo

Marko 14:66—72

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Petro alikosea Bwana wake na akajuta, lakini Yesu alielewa na akamuonyesha upendo kwa kumsameha. Hata sisi tukimkosea mtu kwa matendo au kwa maneno tunapaswa kuomba msamaha wa kweli, na tunaweza kusamehewa.

Maneno maalum

1. Pasaka + Yesu anatabiri + Petro anakana
2. Walinzi wa silaha + chukua Yesu + wanafunzi watoroka + Petro afuata
3. Yesu + Mahakama Makuu + ushahidi wa uongo + Yesu + kifo
4. Petro +chunguza + nje + moto
5. Kijakazi + uliza + rafiki wa Yesu + Petro alikana
6. Petro anaulizwa + mara tatu + alikana Yesu
7. Jogoo awika + Petro anakumbuka + maneno ya Yesu + Petro anasikitika

45.1 Wakati wa chakula cha Pasaka, Yesu alimwambia Petro, “Kutakapokuwa kukipambazuka na kabla jogoo kuwika utanikana mara tatu.”

45.2 Baada ya Yuda kumsaliti Yesu, watu waliokuwa na silaha walienda mbio mbio mitahani na Yesu. Wanafunzi walikuwa na uoga wakatoroka wasijue kitakacho fanyika. Petro alifuata kwa umbali na akaona walikokuwa wakimpeleka Yesu Alihofia kitakacho fanyika kwa Bwana wake aliyempenda. Sawia na kuogopea usalama wake pia.

45.3 Walipeleka Yesu kwa ukumbi wa baraza la Kuhani mkuu. Alikuwa na baraza lake lote kumtafuta Yesu makosa ili wamshitaki. Hapa ndio mahakama makuu ya Wayahudi. Chini ya amri ya Warumi, baraza hili lilipewa mamlaka lakini sio ya kupeana hukumu kubwa. Baraza hili lilitafuta ushahidi wa uongo ili Yesu auwawe.

45.4 Petro aliogopa vile hali ilikuwa ikiendelea. Ilikuwa hatari kwake pia lakini kwa ajili alimjali Yesu alitaka awe huko na asijulikane wakati alipokuwa huko.

45.5 Petro alirandaranda uwanjani mpaka alipohisi baridi akaenda kuota moto. Kijakazi mmoja alipokuwa akipita alimwona na akauliza, “Si wewe ni rafiki wa huyo mtu aliyekamatwa?” “La la umekosea .Sijui wala sielewi unalosema.”



45.6 Mara tatu usiku huo, hilo swali liliulizwa. Kila mara Petro alipeana jibu lile lile. “Sijui huyo mtu. Sijui huyo mtu.” Papo hapo jogoo akawika.

45.7 Bunde tu, Petro alimuona Yesu na macho yao wawili yalikutana labda kupitia kwa dirisha lililokuwa wazi. Kwa ajili ya hiyo Petro alijuta akaangua kilio. Halafu akakumbuka maneno ya Yesu, “Kabla jogoo awike utakuwa umenikana mara tatu.”